**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**OFISI YA WAZIRI MKUU,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MTAA**

# SHULE YA MSINGI MARTIN LUTHER

**P. O. Box 1786 Dodoma. Tel. +255 26 2395029, +255 784 449098**
**Fax +255 26 2395030 (www.martinlutherschooldodoma.sc.tz)**

***"ELIMU BORA ZAIDI KWA KIZAZI KIPYA"***

## DARASA LA IV – HOLDAY PACKAGE

## HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

**JINA LA MWANAFUNZI: ______________________________**

## MAELEKEZO

1. **Kumbuka kuandika majina yako matatu vizuri.**
2. **Jibu maswali yote kulingana na maagizo.**
3. **Soma maswali yote kwa uangalifu kabla ya kujibu.**
4. **Kifurushi hiki cha likizo kinapaswa kurudishwa shuleni tunapofungua.**

**JINA LA MWANAFUNZI** ______________________________ **DARASA LA IV** __________

## SEHEMU A

**1. Jibu vipengele (i) – (xxx) kwa kuchagua jibu sahihi na kuandika herufi yake katika kisanduku ulichopewa.**

i. Kitendo kipi kati ya hivi vifuatavyo ni kinyume na maadili?
   A. Kuheshimiana   B. Matumizi ya madawa ya kulevya
   C. Kukataa rushwa   D. Kushirikiana   [ ]

ii. Kipindi cha zama za mawe za kati kilishuhudia maendeleo gani ya kipekee katika maisha ya binadamu?
   A. Ugunduzi wa moto   B. Makazi ya kudumu
   C. Ugunduzi wa chuma   D. Uvuvi na uwindaji   [ ]

iii. Binadamu wa kale alitengeneza moto kwa kutumia vijiti viwili. Je, kijiti kilichotumika kuchochea moto kilijulikana kwa jina gani?
   A. Ulindi   B. Ulimbombo   C. Uwindi   D. Muanzi   [ ]

iv. Matendo gani kati ya haya si wajibu wa mtoto?
   A. Kufanya usafi binafsi wa mwili na nguo zake
   B. Kutafuta fedha za chakula cha familia nyumbani
   C. Kufanya usafi mahali anapolia chakula
   D. Kusaidia wazazi na walezi kufanya kazi mbalimbali   [ ]

v. Jamii za watanzania zilizingatia maadili katika utoaji wa tiba asili. Ni maadili gani yalizingatiwa katika tiba asili kati ya haya yafuatayo?
   A. Uadilifu, upendo, huruma   B. Uongo, udanganyifu, uoga
   C. Uchafu, ukatili, upole   D. Udanganyifu, ubabaishaji, ulaghai   [ ]

vi. Kusimamia na kulinda haki za Watoto ni wajibu wa nani?
   A. Wazazi na walezi   B. Walimu pekee
   C. Viongozi wa serikali   D. Jamii nzima   [ ]

vii. Miji ipi hapa Tanzania ilikuwa ni maarufu kwa biashara ya utumwa?
   A. Dodoma na Tabora   B. Bagamoyo na Zanzibar
   C. Kibah ana Kilwa   D. Kilwa na Butiama   [ ]

viii. Kusalimiana ni mojawapo ya matendo ya maadili. Zifuatazo ni njia za kusalimiana, ISIPOKUWA

A. Kushikana mikono B. Kupiga goti
C. Kushika Kichwa D. Kupiga makofi [ ]

ix. Habibu ni mtoto wa dada wa baba yangu. Je, ninamwitaje Habibu?

A. Kaka B. Dada C. Mpwa D. Binamu [ ]

x. Jumba lililotumiwa na mfalme au Sultani wa Kilwa kama makazi liliitwaje?

A. Husuni kubwa B. Ngome ya Yesu
C. Caravan Serai D. Azania Front [ ]

xi. Vitu au mambo yenye thamani ambayo tumeyapokea kutoka vizazi vilivyotangulia huitwaje?

A. Makumbusho B. Sanamu C. Urithi D. Historia [ ]

xii. Kuna aina ngapi za urithi?

A. Tano B. Mbili C. Tatu D. Sita [ ]

xiii. Mtoto ana wajibu wa kushiriki katika shughuli za kijamii na taifa lake. Zifuatazo ni shughuli za jamii na taifa ambazo mtoto anaweza kushiriki ISIPOKUWA

A. Shughuli za msiba B. Kupiga kura katika uchaguzi mkuu
C. Ibada na harusi D. Sherehe za kitaifa [ ]

xiv. Kipi kati ya haya yafuatayo siyo miongoni mwa matendo ya kujithamini?

A. Kunawa mikono baada ya kutoka masalani
B. Kuvaa mavazi nadhifu
C. Kutumia mwamvuli wakati wa mvua
D. Kutumia madawa ya kulevya [ ]

xv. Sheria ya mtoto nchini Tanzania ilitungwa mwaka gani?

A. 2009 B. 2014 C. 2013 D. 2019 [ ]

xvi. Kitendo cha kupiga hatua kutoka ngazi ya chini hadi ya juu kimaisha huitwaje?

A. Elimu B. Maendeleo C. Uhuru D. Kutofanikiwa [ ]

xvii. Jambo lipi kati ya haya yafuatayohujenga uhusiano mwema na watu wengine?
A. Kutumia lugha ya upole B. Kutumia lugha ya kejeli
C. Kuwadharau wengine D. Kuwatukana wengine [ ]

xviii. Bendera ya Tanzania ina jumla ya rangi nne. Je, ni rangi gani huonesha uoto wa asili?
A. Kijani B. Njano C. Nyeusi D. Bluu [ ]

xix. Watu waliojihusisha na shughuli za ufugaji wa chuma katika jamii za kitanzania waliitwaje?
A. Wahunzi B. Wahandisi C. Wasusi D. Warugaruga [ ]

xx. Ni urithi upi kati ya hii uliachwa na wamisionari waliotoka nchi za ulaya?
A. Mikuki B. Makanisa
C. Misikiti D. Michoro ya mapangoni [ ]

xxi. Ni tukio gani la kihistoria lilitokea katika nchi yetu mnamo tarehe 9/12/1961?
A. Tanganyika ilipata uhuru B. Nchi ya Tanzania iliundwa
C. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar D. Mapinduzi ya Zanzibar [ ]

xxii. Kitendo cha kuvuka Barabara maeneo yenye alama za pundamilia huashiria nini?
A. Utii wa sheria za shule B. Utii wa sheria za usalama barabarani
C. Kutotii sheria za barabarani D. Kuheshimu haki za Watoto [ ]

xxiii. Bibi yangu anaishi kwenye nyumba ya umbo la mstatili iliyojengwa kwa fito, kukandikwa kwa udongo kisha paa lake kufunikwa kwa udongo. Je, nyumba hiyo inaitwaje?
A. Manyata B. Msonge C. Tembe D. Banda [ ]

xxiv. Elimu ya maadili ya afya ya uzazi kwa vijana iliyotolewa kabla ya ukoloni ilijulikana kama
A. Unyago na ususi B. Ufinyanzi na jando
C. Ususi na uhunzi D. Jando na unyago [ ]

xxv. Rushwa ni adui wa haki, ndio maana Tanzania imeundwa Taasisi maalumu ya kuzuia kitendo hicho. Taasisi hiyo ni ipi?
A. TANAPA B. Katiba C. Benki kuu D. TAKUKURU [ ]

xxvi. Neno mtemi lilitokana na neno “kutema”lenye maana ya kukata/ kufyeka mapori ili kuongeza himaya. Utawala wa watemi ulianza katika jamii zipi hapa nchini?
A. Wahehe B. Wanyamwezi C. Wanyaturu D. Wahaya [ ]

xxvii. Uvumbuzi wa zamadamu ulifanyika katika bonde la Olduvai mkoani Arusha. Je, fuvu hili la zamadamu lilivumbuliwa mwaka gani?
A. 1964 B. 1961 C. 1957 D. 1959 [ ]

xxviii. Taaluma ya uchunguzi wa kisayansi kuhusu masalia ya mambo ya kale na utamaduni wa binadamu huitwa?
A. Makavazi B. Akiolojia C. Sayansi D. Makumbusho [ ]

xxix. Mfumo uliotumiwa na jamii ya wahaya kumiliki ardhi kipindi cha ukabaila ulijulikana kama
A. Unyarubanja B. Umwinyi C. Ubugabire D. Utemi [ ]

**2. Kwa kipengele cha (i- v) oanisha sehemu "A" na maneno yaliyopo sehemu "B" kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.**

| ORODHA "A" | MAJIBU | ORODHA "B" |
|---|---|---|
| i. Mtemi Mkwawa | | A. Wahaya – Kagera |
| ii. Mtemi Mirambo | | B. Wachaga – Kilimanjaro |
| iii. Mangi Sina | | C. Wangoni – Ruvuma |
| iv. Mtemi Rumanyika | | D. Wahehe – Iringa |
| v. Mtemi Litti Kidanka | | E. Wanyamwezi – Tabora |
| | | F. Wanyaturu – Singida |

**3. Oanisha orodha "A" na orodha "B" katika jedwali na kisha Andika herufi ya jibu sahihi kwenye nafasi ya majibu uliyopewa.**

| ORODHA "A" | MAJIBU | ORODHA "B" |
|---|---|---|
| i. Nyavu | | A. Utengenezaji wa vitu kwa kutumia udongo wa mfinyazi. |
| ii. Ufinyazi | | B. Ulisaidia shughuli za kilimo,uvuvi na uwindaji kukua kwa kutengeneza vitu kama majembe, mishale na ndoano. |
| iii. Ususi | | C. Kifaa chenye matundu kilichosukwa nyuzi kitumikacho katika uvuvi. |

| | | |
|---|---|---|
| iv. Uhunzi | | D. Utengenezaji wa vitu kwa kutumia udongo tu |
| v. Utengenezaji wa chumvi | | E. Ulihusisha kutumia matete, makuti na mianzi kutengeneza vitu kama mikeka, vikapu na nyundo. |
| | | F. Ulifanyika hasa katika maeneo yenye maji ambayo yana asili ya chumvi. |

**4. Oanisha maneno kutoka sehemu "A" na maneno yaliyopo sehemu "B" kisha Andika herufi ya jibu sahihi katika nafasi uliyopewa.**

| ORODHA "A" | MAJIBU | ORODHA "B" |
|---|---|---|
| i. Mwalimu Julius Nyerere alichaguliwa kuwa raisi wa kwanza | | A. 26/04/1964 |
| ii. Kukazama kwa meli ya MV. BUKOBA | | B. 1962 |
| iii. Muungano wa Tanga nyika na Zanzibar | | C. 09/12/1961 |
| iv. Uhuru wa Zanzibar | | D. 10/12/1963 |
| v. Tanganyika ilipata uhuru | | E. 1996 |

**5. Kwa kipengele cha (i-v) chagua majibu katika jedwali kisha uyaandike katika nafasi zilizoachwa wazi.**

| |
|---|
| Kamati ya shule, Mwalimu, Mwalimu mkuu, viranja, Mwalimu wa nidhamu, Mwalimu wa taaluma |

i. Tunawaongoza wanafunzi wenzetu katika kukuza na kutunza maadili mema sisi ni akina nani? ______________________________

ii. Huongozwa na wazazi ambao wamechaguliwa na wazazi wenye Watoto katika shule husika mimi ni nani? ______________________________


iii. Mimi ndiye katibu wa kamati ya shule pia husimamia taaluma na nidhamu ya wanafunzi wote shuleni. Mimi ni ________________________

iv. Husimamia na kufuatilia maadili na taaluma shuleni katika ngazi mbalimbali mimi ni nani? _________________________

v. Mimi ni kiongozi mkuu wa kusimamia maadili shuleni unafikiri nitakuwa nani? __________________

6. **Jibu maswali kipengele cha (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano.**
   i. Mchezo wa asili unaotumia nguvu ________________________(mieleka, mdako, bao)
   ii. Maarifa na ujuzi wa asili katika utayarishaji wa dawa za asili ulifanyika kwa ____________________________(kuchemsha, kunywa, kuoga)
   iii. Miti midogo mirefu mfano wa fimbo zilizosukwa kwa kamba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za asili ________________________( mianzi, fito, makuti)
   iv. Kutandaza au kuweka kitu kwenye mwanga wa jua au upepo kwa lengo la kukausha _____________________(anika, banika, finyanga)
   v. Vitu vilivyochongwa mfano wa Wanyama au binadamu kwa kutumia miti _____________________________(ukili,vivyago, dau)

7. **Chunguza kielelezo kifuatacho kisha jibu maswali kipengele cha (i-iv) kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**




**Maswali.**

i. Herufi A inawakilisha viongozi gani? ___________________________


ii. Herufi B inatoa tafsiri ya mnjama. Je, inatakiwa iandikwe nini? _____________________________

iii. Kabila linalowakilishwa na mfumu huo hapojuu lilikuwa maarufu katika shughuli ipi kabla ya ukoloni? ______________________________

iv. Je, ni ngoma ipi ya jadi ya kabila lililotumia mfumo huo wa uongozi?

___________________________


8. **Chunguza kwa makini kielezo kifuatacho na kisha jibu maswali yafuatayo kipengele cha (i-iv) kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**




**Maswali.**

i. Kielelezo kilichooneshwa hapo juu kinawakilisha nini? ______________________________
ii. Ni uhusiano wa aina gani umeoneshwa katika kielelezo hapo juu? __________________________
iii. Shadrack na Musa wanamuitaje Maria? ___________________________________
iv. Musa anamuitaje Joachim? _____________________________


9. **Chunguza kielelezo kifuatacho kwa umakini kisha jibu maswali kipengele cha (i-vi) kwa kujaza jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.**



**Maswali.**

i. Kielezo hiki kinaonesha nini? ____________________________
ii. Kabila gani lilitumia mfumo uliooneshwa hapo juu? __________________________
iii. Pendekeza ngoma ya asili ya kabila hilo? ________________________________
iv. Katika maneno yaliyoandikwa kwenye mfumo huo neno lipi huwakilisha mkutano wa wazee wa ukoo? ___________________________


**10. Kwa kipengele cha (i-v) chunguza picaha ifuatayo kwa umakini kisha jibu maswali kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**



**Maswali.**

i. Shughuli ya ki Uchumi iliyooneshwa kwenye picha inaitwaje? ___________________________
ii. Taja jamii(2) mbili zilizojishughulisha na shughuli hii kabla ya ukoloni
   a) ______________________________________________
   b) ______________________________________________
iii. Pendekeza bidhaa (2) mbili zilizotengenezwa katika shughuli uliyoitaja
   a) _____________________________________________
   b) _____________________________________________
iv. Udogo wenye chembechembe za madini ya chuma uliochimbwa ardhini ili kuwekwa kwenye tanuru uliitwaje? _______________________________
v. Udongo ulipoyeyuka ulijitenge na maji maji ya chuma yaliyoganda katika tanuru. Majimaji hayo yalijulikana kama _________________________

**11. Jibu maswali kwa usahihi kulingana na picha uliyopewa. Chunguza picha kwa makini.**



**Maswali.**

i. Picha hapo juu inaonesha shughuli gani ya Uchumi inayofanyika?
_____________________________

ii. Taja kifaa kimoja kinachitumika katika shughuli inayofanyika hapo juu?
_________________________

iii. Taja faida moja ambayo wanaipata watu ambao walijishughulisha na shughuli hiyo
______________________

iv. Ni maeneo yenye upatikanaji wa nini hasa amabako shughuli hiyo inaweza kufanyika
_______________________

v. Taja shughuli nyingine ya Uchumi au uzalishaji amabayo inaweza kufanyika Tanzania____________________

**12. Chunguza kwa umakini picha ifuatayo kisha jibu maswali kipengele cha (i-v) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.**



**Maswali.**

i. Alama gani katika picha hii huashiria uwepo wa rasilimali za madini nchini?
____________________________

ii. Taja mazao mawili ya biashara yanayooneshwa na picha hapo juu
   a) ______________________________
   b) ______________________________

iii. Mwenge wa uhuru ni mojawapo ya alama zilizopo katika picha hapo juu. Je, uliwashwa kwa mara ya kwanza lini? _______________________________________

iv. Alama ipi katika picha hapo juu kuwakilisha rasilimali za maji? ________________________

v. Ni nani aliyebuni alama ya taifa inayoonekana katika picha hapo juu______________________

**13. Umepewa sentensi sita (i-vi) ambazo zimechanganywa zipange katika mtiririko ulio sahihi kwa kuzipa herufi A, B, C, D, E na F.**

i. Hii ilisababisha binadamu kufanya majaribio zaidi ya utengenezaji wa moto [ ]
ii. Binadamu alipokuwa akitengeneza zana aligundua uwepo wa cheche za moto wakati akigongagonga na kusugua mawe [ ]
iii. Binadamu alianza kwa kupekecha vijiti viwili vikavu ili kupata moto [ ]
iv. Baada ya kupata moto binadamu alianza kula vyakula vilivyopikwa, kubanikwa aua kuchomwa [ ]
v. Pia binadamu Aliona cheche za moto zilizotokana na radi wakati radi ilipopiga [ ]
vi. Sayansi na teknolojia ya kutengeneza moto iligundulika katika harakati za utengenezaji wa zana [ ]

**14. Soma kwa makini kifungu cha Habari kifuatacho kisha jibu kipengele (i-vi).**

Kingu ni mtoto wa kwanza katika familia ya Rushashele. Mama yake ni Hidaya. Kingu ana kaka wawili na dada watatu. Kaka zake ni Kamleti na Kipala. Kingu amemuoa Zena. Kaka zake wameoa pia. Kamleti amemuoa Dengue na kipala amemuoa Dumeka . Dada zake Kingu ni Lushaina, Halima na Bhoke. Wote wameolewa katika familia mbalimbali. Kwa hiyo Kingu, baba yake, kaka zake wawili, dada zake watatu, Watoto wake wa kike na wakiume wote ni wa ukoo mmoja.

Kingu na mke wake wanawatoto watatu. Majina yao ni Zabedayo, Hamisa na Karomo. Hamisa ameolewa na Hatibu na wana watoto wawili ambao ni Swedina Zuhura .

**Maswali.**

i. Rushashele na Hidaya wana wajukuu wangapi? ________________________________
ii. Hatibu anamwitaje Kingu __________________________
iii. Swedi anamuitaje Zebedayo _______________________
iv. Bhoke anamuitaje Dumeka? __________________________

v. Dumeka anamwitaje Kingu ______________________

**15. Panga viongozi wa shule wafuatao katika mtiririko sahihi kuanzia ngazi ya juu kabisa ya uongozi hadi ngazi ya chini kabisa kwa kutumia herufi (A-F) kipengele cha (vii) kimefanyika kama mfano**

i. Mwalimu mkuu msaidizi [ ]
ii. Kamati ya shule [ ]
iii. Mwalimu mkuu [ ]
iv. Mwalimu wa nidhamu [ ]
v. Walimu [ ]
vi. Mwalimu wa taaluma [ ]
vii. Viranja [ **G** ]